



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE

KATIKA JIMBO LA BABATI MJINI NA UKEREWE PAMOJA NA

UDIWANI KATIKA KATA 26 ZA TANZANIA BARA

Tume ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi ya Ubunge katika Majimbo mawili (2), **Jimbo la Babati Mjini lililopo Halmashauri ya Mji wa Babati Mkoani Manyara na Jimbo la Ukerewe katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe Mkoani Mwanza.** Nafasi hizo wazi zimetokana na waliokuwa Wabunge wa Majimbo hayo Bwana. Joseph Michael Mkundi na Bi. Pauline Philipo Gekul kujiuzulu kutoka kwenye Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Vile vile, Tume imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ambaye kwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata 26 za Tanzania Bara. Nafasi hizo wazi zimetokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo na kujiuzulu.

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 37 (1) (b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, pamoja na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa Umma kuhusu uwepo wa Uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Majimbo ya Babati Mjini na Ukerewe pamoja na Udiwani katika Kata Ishirini na Sita (26) za Tanzania Bara.

Uchaguzi huu mdogo katika Majimbo ya Babati Mjini na Ukerewe **utafanyika sambamba na uchaguzi katika Majimbo ya Serengeti, Simanjiro pamoja na Kata 21** zilizotangazwa awali kwa Ratiba ifuatayo:

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe 28 Oktoba hadi 3 Novemba mwaka huu;
2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 3 Novemba mwaka huu;
3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 4 Novemba hadi tarehe 1 Desemba mwaka huu; na
4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe 2 Desemba, mwaka huu

Tunapenda kuvikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha Uchaguzi huu mdogo.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Imetolewa leo tarehe 17 Oktoba, 2018.

Mhe. Jaji (R) Mbarouk S. Mbarouk  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## KATA ZILIZOWAZI

NA	MKOA	HALMASHAURI	NA	KATA
1	DAR ES SALAAM	HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE	1	MTONI
		HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA	2	MNYAMANI
2	DODOMA	HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA	3	SALANKA
3	MWANZA	HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU	4	KABILA
		HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI	5	SUMBUGU
			6	BUHINGO
		HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE	7	BUKIKO
4	LINDI	HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA	8	MITEJA
			9	KIVINJE SINGINO
			10	SOMANGA
			11	MITOLE
5	RUVUMA	HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA	12	MATARawe
			13	RUVUMA
		HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA	14	MTIPWILI
		HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU	15	NALASI MASHARIKI
	MARA	HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA	16	KASUGUTI
			17	BUTIMBA
				HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI

NA	MKOA	HALMASHAURI	NA	KATA
6			19	RING'WANI
			20	RUNG'ABURE
			21	NATTA
			22	RIGICHA
7	MANYARA	HALMASHAURI YA MJI WA BABATI	23	MAISAKA
8	ARUSHA	HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU	24	NKOANEKOLI
9	NJOMBE	HALMASHAURI YA MJI WA MAKAMBAKO	25	MJIMWEMA
10	PWANI	HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI	26	SALALE